**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI, MHE. MHANDISI BALOZI JOHN W. H. KIJAZI KUHITIMISHA MATEMBEZI YA WATUMISHI WA TAASISI ZINAZOSIMAMIA MAADILI, UWAJIBIKAJI, UTAWALA BORA, HAKI ZA BINADAMU NA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA, TAREHE 3 DESEMBA 2016.**

***Bw. Peter A. Ilomo, Katibu Mkuu, IKULU;***

***Bw. Valentino Mlowola, Mkurungenzi Mkuu wa TAKUKURU na Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Maadhimisho ya siku hii ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa;***

***Wakuu wa Taasisi zinazosimamia Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji na Mapambano dhidi ya Rushwa;***

***Ndugu Viongozi mbalimbali wa Serikali;***

***Wawakilishi wa Asasi za Kiraia;***

***Wageni waalikwa;***

***Waandishi wa Habari;***

**Mabibi na Mabwana;**

**<u>Habari za Asubuhi!</u>**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki kwenye matembezi haya muhimu siku ya leo. Nichukue fursa hii kuwashukuru Waandaaji wa matembezi haya kwa maandalizi yao mazuri na mwaliko wa kushiriki nanyi. Hakika nimefarijika sana. Matembezi haya ni muendelezo wa Kampeni ya Kitaifa ya mwezi mmoja kuhusu **"Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa".** Kampeni hii ambayo uzinduzi wake ulifanyika tarehe 10 Novemba 2016, imepangwa kuhitimishwa siku ya kilele cha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu nchini, yaani tarehe 10 Desemba 2016.

**Ndugu Wananchi;**

Matembezi ya hiari tuliyoyafanya leo ni muhimu sana kwetu, kwani yameimarisha afya zetu, hivyo kutuweka katika hali nzuri zaidi ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya ujenzi wa taifa, ikiwa ni pamoja na kuzingatia maadili kwa kiwango cha hali ya juu. Wote tunatambua kuwa Taifa imara hujengwa na wananchi imara, wenye afya njema. Kwa hiyo wito wangu kwetu sote ni kuwa, tuendeleze utamaduni wa kufanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha afya zetu na kujijengea uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiafya na nyingine za kimaisha.

Matembezi haya pia yanaashiria mshikamano ambao unapaswa kuwepo miongoni mwa Taasisi zote zinazoshiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini. Mshikamano huu haupaswi kuishia

kwenye Taasisi hizi pekee, bali vilevile Asasi za Kiraia na Kidini, Taasisi za Elimu, Wanahabari na wananchi wa kawaida wote ni wadau muhimu katika mapambano haya. Hivyo, nimefarijika sana kuona matembezi haya kwa mara ya kwanza yamewakutanisha watumishi wote wa Ofisi na Taasisi zinazosimamia Maadili, Uwajibikaji, Utawala Bora, Haki za Binadamu na Mapambano dhidi ya Rushwa nchini. Taasisi hizo ni pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU); Ofisi ya Rais - Utumishi na Utawala Bora; Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali; Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA); na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Naamini wote tumepata fursa ya kubadilishana mawazo na kujenga mahusiano ya karibu wakati ya matembezi haya. Mahusiano baina ya taasisi zetu ni muhimu katika utekelezaji wa malengo yetu ya pamoja kitaifa, ambayo ni **kujenga maadili**, **haki za binadamu**, **uwajibikaji**, **utawala bora** na **kutokomeza rushwa na ufisadi**.

**Ndugu wananchi;**

Mtakumbuka kuwa, tarehe 9 Desemba kila mwaka Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) huadhimisha *Siku ya Kimataifa ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa* (*International Anti-Corruption Day*). Nchi Wanachama ni zile zilizosaini na kuridhia *Mapatano ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2003 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa* ya mwaka 2003. Mapatano haya yalisainiwa tarehe 9 Desemba, 2003 huko Merida, Mexico na yalianza kutumika rasmi kisheria kuanzia tarehe 14 Disemba, 2005 baada ya kuridhiwa na nchi zaidi ya 30. Tanzania iliridhia Mapatano haya tarehe 25 Mei, 2005. Hii yote ni katika kudumisha uumini wa nchi yetu katika falsafa ya Uwazi, Uwajibikaji, Haki za Binadamu na Utawala Bora ambavyo vimedumu tangu kuzaliwa kwa Taifa huru la Tanzania.

Tangu iridhie mapatano hayo, Tanzania imekuwa ikiungana na nchi nyingine zilizoridhia na kuadhimisha siku hii. Hata hivyo, maadhimisho hayo yamekuwa yakifanyika tarehe 10 Desemba ya kila mwaka na kutambulika kama "Siku ya Maadili Kitaifa", badala ya tarehe 9 Disemba, kwani ni siku ambayo imetengwa mahsusi kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Tanzania (Bara).

**Ndugu wananchi;**

Tanzania pia inaunga mkono, **"Tamko la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu** (Universal Declaration on Human Rights)" lililopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1948**.** Kufuatia tamko hilo, ambalo limetafsiriwa katika Mikataba ya Kimataifa na Katiba za nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania, tarehe 10 Disemba ya kila mwaka, Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa huadhimisha **"Siku ya Haki za Binadamu."** Kauli mbiu ya maadhimisho ya siku hiyo kwa mwaka huu ni "Stand up for someone's rights today", ikiweka msisitizo kuwa **kila mmoja wetu anayo haki na wajibu wa kulinda, kutetea na kutoathiri upatikanaji wa haki kwa wengine**. Serikali ya Tanzania itaendelea kuhakikisha kuwa wananchi wote, bila kujali itikadi zao, dini zao ama uwezo wao kiuchumi, kielimu n.k. wanafaidi haki za msingi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ndugu wananchi;**

Madhumuni ya Tanzania kushiriki katika kuadhimisha **Siku ya Maadili na Haki za Binadamu** ni kuliwezesha Taifa letu kuudhihirishia ulimwengu dhamira yake ya dhati ya kusimamia kwa vitendo dhana na misingi ya uadilifu, haki za binadamu, utawala bora, uwajibikaji, mapambano dhidi ya rushwa, kuimarisha nidhamu katika Utumishi wa Umma na kuongeza kasi ya maendeleo kwa Taifa letu. Madhumuni mengine ni kuikumbusha na kuihamasisha jamii nzima kujua haki zao na wajibu wao kama raia; na kuwaunganisha wananchi wote kukusanya nguvu zao pamoja ili kuhakikisha kuwa wanapambana na kukabiliana na changamoto mbalimbali za Maadili, Rushwa na Haki za Binadamu zilizopo. Makundi haya ni pamoja na Viongozi wa Serikali na Siasa, Watumishi wa Umma, Vyombo vya Habari, Taasisi za Dini, Asasi za Kiraia na Wananchi kwa ujumla.

**Ndugu wananchi;**

Kwa kuwa suala la maadili ni mtambuka na linamgusa kila mtu, ninatoa wito kwa Taasisi zote za Umma, Sekta Binafsi na makundi mbalimbali katika jamii kuwa chachu ya kuliwezesha Taifa letu kutekeleza na kusimamia kwa vitendo dhana ya Uwajibikaji, Uadilifu, Haki za Binadamu, Utawala Bora, na Mapambano Dhidi ya Rushwa. Ikumbukwe pia, kwamba maadili ni pamoja na kujali haki za watu wengine.

Maadili yana umuhimu mkubwa katika utawala na maendeleo ya nchi, kwani huleta matokeo chanya. Baadhi ya matokeo hayo ni pamoja na:

1) Kusaidia kujenga imani ya wananchi kwa Viongozi na Serikali kwa ujumla;
2) Kusaidia kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa maslahi ya wote;
3) Kusaidia kuongeza tija na thamani ya huduma zinazotolewa na Serikali;
4) Kusaidia kudhibiti mianya ya vitendo vya rushwa;
5) Kusaidia kujenga ujasiri wa kusimamia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma;
6) Kuwezesha wananchi, Viongozi na Watumishi wa Umma kutoa mchango mkubwa na wa haraka katika utekelezaji wa maendeleo ya nchi;
7) Kuepusha utata wa maamuzi au mgongano wa maslahi;
8) kuwezesha kuweka mazingira chanya ya uwekezaji;
9) Kujenga na kudumisha amani, utulivu, kuheshimiana na umoja wa kitaifa; na
10) Kuondoa hulka ya ubinafsi kwa Viongozi na Watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla.

**Ndugu Wananchi,**

Napenda nizungumzie suala la **Hulka ya Ubinafsi** ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa katika vitendo vya rushwa na ufisadi. Ipo mifano ya sehemu ambazo rushwa imekithiri kutoka katika ngazi ya juu kabisa ya Taasisi hadi ile ya chini, kwa sababu ya ubinafsi na uroho wa watendaji. Mtumishi wa Chini anakula rushwa kwa vile mkubwa wake anafanya hivyo. Kadhalika mkubwa hawezi kumsimamia mdogo kama Sheria ya Maadili inavyomtaka kwa kuwa yeye mwenyewe mikono yake si misafi. Matokeo yake hata awe na mali nyingi kupindukia, bado ataendelea kula rushwa bila kikomo.

Ndio maana Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kwa dhati kabisa kupambana na rushwa za kila aina kwa lengo la kujenga jamii yenye maadili na inayochukia vitendo vya rushwa na ufisadi. Jitihada za serikali ni kuondokana na **Hulka ya Ubinafsi na Uroho** na badala yake kujenga utamaduni na tabia ya kujitolea (**What can I give spirit**) katika jamii yetu. Mifano ya utekelezaji wa jambo hili ipo mingi, lakini ulio dhahiri ni wa Kampeni ya kuchangia madawati, ambayo imefanyika kwa ufanisi mkubwa nchini kote. Naamini kuwa tukiendeleza utamaduni huo wa kizalendo, nchi yetu itapiga hatua kubwa zaidi na kwa kasi.

**Ndugu wananchi;**

Kwa kumalizia, ninatoa pia wito kwa waandishi wa habari na vyombo vya habari kwa ujumla kuendelea kuonyesha uzalendo katika kipindi chote cha kampeni hii, kwa kuielimisha jamii kuhusu **"Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji, Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa".** Tunawaomba mzidi kutumia taaluma zenu na vyombo vyenu kuwahabarisha na kuwahamasisha wanajamii juu ya yale yatakayokuwa yanafanyika katika kipindi hiki cha kampeni, pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa na kuzingatia misingi ya uadilifu, haki za binadamu, uwajibikaji na utawala bora katika maisha yao ya kila siku.

Nazishukuru tena Taasisi zote zilizoandaa Kampeni hii kwa kunipa nafasi ya kushiriki katika matembezi haya kama sehemu ya maadhimisho ya Siku **ya Maadili na Haki za Binadamu**. Nawaomba muendelee kushiriki kwa vitendo katika kampeni mliyoianzisha, na ushirikiano huu uendelezwe ili kufanikisha malengo yenu na hivyo kuwezesha Taifa kunufaika na utendaji wenu katika maeneo yenu ya kazi.

***Mungu Ibariki Tanzania,***

***Mungu Ibariki Serikali yetu,***

***Ahsanteni kwa Kunisikiliza.***